**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**13 Septemba 2008**

**Waliohudhuria**
Alen J Nyanginywa
Ally Athuman Jumbe
Ally Mzee Amiri
Ally Saidi Mwishehe
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Chichi Iddy
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Kibwana Mohammad Msiga
Mejah Mbuya
Mussa Alex
Paulo Atibu Hatibu
Shamte J Kigoma
Shukuru Hassan
Tomassi Sabinussi

**Wamba Memorial Fund – Mradi wa Usalama Barabarani**
Mejah alisema aliongea na Mama Wamba, mama wake Phillipe Wamba, ambaye Mejah alimfahamu. Tulikubali kumwalika kwenye mkutano wa UWABA, labda tarehe 4 Oktoba.

**Kibwana**
Kibwana alitumia Tsh 35,000 kununua mipira na breki kwa baisikeli yake. Kwa sababu hajakutana na Hussein Hamza aliomba fundi mwingine kufanya kazi na atamaliza hapo karibu.

**Kongamano**
Jumatano Elaine, Juma Jongo na Juma Chibaya walienda kumwona Diwani Lupilya kueleza kuhusu kongamano. Alipenda wazo hili na alisema atafuatalia na watu wanohusika serekali ya jiji na atatupa jibu.

Azzan Zungu yupo Dodoma lakini atarudi wiki ijayo. Mejah na Juma wataenda kumwona.

**Umoja wa Ulaya**
Elaine alileta email tuliyopata kutoka umoja wa Ulaya.

Kufuatalia tulikubali:

- Kuomba mkutano na Tanzania Roads Association TARA, ambayo EU walisema ni shirika la washika dau
- Kuandika barua kwa wizara ya miundombinu kuomba kuwa kwenye orodha ya washika dau ya miradi ya barabara, kwa sababu EU wanasema kuna orodha kama hiyo. Pia kuomba mkutano na Waziri mpya Shukuru Kawambwa
- Kuandika barua kwa EU kuomba waandike sera kuhusu usafiri wa siyo ya moto, kwa sababu wanasema hawana sera kama hiyo sasa.
- Kuendesha baisikeli kwenye barabara ya Nelson Mandela Road kutoa repoti kama kuna service roads na kama kuna vizuio kuepuka magari kutumia service roads, kama EU walisema

**Msafara wa Baisikeli**

Mejah alipendekeza tuombe udhamini kutoka British High Commission pia.

Ubalozi wa Uholonzi walisema kwa email kwamba hawataweza kudhamini mwaka huu na walipendekeza tujaribu ubalozi wa Norway.

Elaine alimpigia simu Bwana Abdul wa Bakhresa na alisema hajaona barua yetu. Juma alimpeleka nakala nyingine kwake mwenyewe na alisema atafuatalia na Bwana Bakhresa na atatupa jibu.

Diwani Lupilya alipendekeza tuandika barua kwa Serengeti Breweries na yeye atawaletea kwa ajili yetu. Bada ya hapo Juma alimpa barua kwenda kwa Serengeti Breweries.

Juma pia alipeleka barua kwa ubalozi wa China wiki hii.

Mejah na Juma watafuatalia na simu na kwa kutembelea maofisi wiki hii – ubalozi wa Ireland, ubalozi wa China, CRDB, NMB, Bakhresa, Ultimate Security na kampuni ya guta.

Mejah na Juma pia watamtembelea Azzan Zungu kufuatalia barua kuomba yeye awe mgeni rasmi, na watafuatalia barua ya manispaa ya Ilala kuomba kutumia uwanja wa Mnazi Mmoja.

Tuliongea kuhusu njia ya msafara na Elaine alisema kwamba ni muhimu iwe mfupi kwa sababu tutakuwa na walemavu na watoto.

**Mkutano wa gTKP Cameroon**

Wakati wa wiki Elaine na Mejah waliandia maada kwa Mejah kutoa kwenye mkutano wa Cameroon. Tuliongea kuhusu maada na tulifanya marekebisho.

**Traffic Police**

Mejah na Husein Hamza walisikia kwenye TV na redio (Radio Taifa) matangazo kuhusu usalama barabarani na matumizi ya service roads. Juma alipeleka barua yetu kwa traffic police.

**Daraj la Kigamboni**
Juma alipeleka barua kuhusu daraja la Kigamboni kwa NSSF.

**Utafiti wa mwanafunzi wa Rwanda Alphonse Mkurunziza**
Elaine alisema kwamba mwanafunzi kutoka Rwanda anafanya utafiti wa PhD kuhusu masuala ya baisikeli Afrika Mashiriki, na atafika leo jioni na ndege. Yeye na Juma wataenda kutana naye kesho asubuhi. Watamwalika kwenye mkutano wa UWABA wa wiki ijayo kuona vipi tunaweza kushirikiana.

**Foundation for Civil Society**
Kwa bahati tulisikia kuhusu Foundation for Civil Society kutoka asili tatu – Mejah aliona programu kwenye ITV ijumaa, road fund walipendekeza tuombe hela ya watu wa zaida kwenda Cameroon na Ubalozi wa Uholonzi walipendekeza tuombe fedha ya msafara wa baisikeli. Elaine aliangalia website na aliwatumia email na mtu kutoka foundation alimpigia simu. Ni mfumo uliyoanzishwa na kundi ya bilateral donors kusaidia civil society. Kuna taratibu malaamu kuomba fedha ambayo inachukua muda na tumeshachelewa kupata hela ya Cameroon wala msafara. Tulikubali kutana nao kuongea kuhusu vipi tunaweza kushirikiana kwenye miradi mengine.

**Mambo ya hela**
Juma alitumia Tsh 800 kwa photocopying. Ally Saidi Mwishehe alileta Tsh 14,000 ya hela ya guta. Ilikuwa wiki tano tangu alileta hela. Aliomba tumsamehe ya wiki mbili kwa sababu ya matatizo alikuwa nayo ya guta yake binafsi kuibiwa na simu kuibiwa, na wanachama walikubali. Basi bado yupo wiki moja nyuma katika malipo. Tulimpa Mejah Tsh 10,000 kupiga simu kufuatalia kuhusu msafara wa baisikeli na tulitumia Tsh 3,000 kununua photos za msafara wa mwaka jana Juma anabaki na Tsh 41,900 ya hela ya UWABA.

Juma Jongo aliomba advance ya posho yake na Juma Chibaya aliomba advance ya kodi ya ofisi. Tulikubali kwamba tutaangalia balansi ya benki na kupiga hesabu hela gani ni ya mradi wa Wamba na hela gani inabaki kwa mambo mengine halafu tutafanya uamuzi..

**Mambo mengine**
Alen aliyejiunga na UWABA leo na pia ni mwanachama wa CHABADA alitangaza kwamba tarehe 5 Oktoba kutakuwa na mashindano ya baisikeli ya Dar es Salaam na tarehe 19 kutakuwa na mashindano Mwanza. Alileta photos za msafara wa mwaka jana alizonunua kutoka mpiga picha na tuliamua kuzinunua kutoka kwake.

Paulo alitembelea HUWATA wakati wa wiki kuongea nao kuhusu shughuli zetu.

Elaine alisema aliongea na mtu aliyependekeza kwamba guta inabeba uzito wake juu sana na ingekuwa bora kuwa na baisikeli na trailer nyuma kubeba bidhaa. Wanachama wengine walisema baisikeli ya kawaida haina nguvu kubeba mizigo mikubwa na guta ni imara sana.